# BRAINWAVE K.C.P.E EXAMINATION PANEL

## DARASA LA NANE

## MWAKA 2022

**003**

BRAINWAVE PUBLISHERS

## — KISWAHILI —

**Muda :Saa 1 Dakika 30**

---

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatsi ya majibu.

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba ako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B,D na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hili.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali:**

21. Nafasi iliyotengenezwa ukutani ili kuwekea vitu ni:-
    A. sefu
    B. shubaka
    C. rafu
    D. kabati

Jibu sahihi ni **B** (shubaka)
Katika karatasi ya majibu

**20.** [A] [B] [C] [D]  **21.** [A] [B] [C] [D]  **22.** [A] [B] [C] [D]  **23.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku ulivyopewa.

**Kitabu jhiki cha maswali kila kurasa 8 zilizopigwa chapa**

Teacher.co.ke

**Kutoka nambari 1 -15. Chagua jibu sahihi kujaza vihasho.**

Usafi ___1___ mazingira ni suala ___2___ kutekelezwa na kila ___3___ anayeipenda nchi ___4___ . Maradhi ___5___ huletwa na uchafuzi wa mazingira ___6___ . Mathalan, ___7___ husababisha malaria. Mbung'o nao huleta ___8___ . Kila apendaye afya njema ___9___ kuhakikisha mazingira yake ni ___10___ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. ya | B. wa | C.za | D. la |
| **2.** | A.lifaalo | B. linaofaa | C.lifaalo | D. linalifa |
| **3.** | A. mzalendo | B. umma | C. moja | D. yoyote |
| **4.** | A. lake | B. kwake | C. mwake | D. yake |
| **5.** | A. mingi | B. mengi | C. nyingi | D. jingi |
| **6.** | A. sheshe | B. haba | C. sugu | D. safi |
| **7.** | A. mbu | B. chafua | C. nzi | D. rubaa |
| **8.** | A. malaria | B. kichocho | C. tauni | D. malale |
| **9.** | A. ana budi | B. hana budi | C. hataki | D. hapendi |
| **10.** | A. safi | B. masafi | C. chafu | D. machafu |

Sudi hakujua ___11___ ya ukaidi hadi ___12___ na maafa. Alikuwa na ___13___ ya kupuuza ushauri wa walimu. Alipofanya mtihani hakuweza ___14___ . Hapo ndipo alipogundua kuwa ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. thamani | B. hasara | C. uzuri | D. mema |
| **12.** | A. alipofikwa | B. alipofuzu | C. aliposikia | D. alipokabili |
| **13.** | A. mila | B. tamaduni | C. ada | D. mazoea |
| **14.** | A. kula mwata | B. kujitoa mhanga | C. kufua dafu | D. kushika tariki |
| **15.** | A. bidii hufaidi | B. Asiyesikia hulia | C. chema hakidumu | D. Akiba haiozi |

Teacher.co.ke

**Kutoka swali la 16- 30, chagua jibu sahihi.**

16. *Chagua wingi wa sentensi ifuatayo.*

Karai husafishwa na dobi yule.

A. Makarai husafishwa na madobi wale.

B. Karai husafishwa na dobi wale.

C. Makarai husafirshwa na dobi wale.

D. Karai husafishwa na madobi wale.

17. Sayari kubwa zaidi kuliko zote huitwa

A. Zohari

B. Kausi

C. Mshatarii

D. Mirihi

18. Nomino mbeleko, mbavu na ndevu hupatikana katika ngeli ya

A. I-ZI

B. U-ZI

C. I-I

D. U-U

19. *Chagua udogo wa sentensi ifuatayo.*

Kiti cha mti huu ni kizuri sana.

A. Kiti cha kijiti hiki ni kizuri sana.

B. Kijiti cha kimti hiki ni kizuri sana.

C. Jikiti cha kijiti hiki ni kizuri sana.

D. Kijikiti cha kijiti hiki ni kizuri sana..

20. *Chagua jibu lenye amri*

A. Nendeni mkawaite wazazi wenu.

B. Meza tembe mbili kila siku.

C. Hamadi ! Umeumja ? Pole sana.

D. Ushikwapo shikamana.

21. Malipo ya kuanzisha biashara huitwa

A. koto

B. mtaji

C. kishanzu

D. faida

22. Nyambua kitenzi <u>fungua</u> katika kauli ya kutendana

A. fungua

B. fungana

C. funguliana

D. funguana.

23. Chagua sentensi yenye '**<u>ni</u>**' ya mtendaji

A. Bustani yetu imenawiri.

B. Mwanafunzi aliingia bweni**ni**.

C. Nilisoma hadithi ya kuvutia.

D. Walimu wameketi majilisini.

24. ***Tegua kitendawili***

Amesimama mbali nyikani lakini aonekana.

A. moto

B. moshi

C. twiga

D. mti

25. Neno wanariadha lina silabi ngapi?

A. 6

B. 5

C. 7

D. 10

26. ***Chagua sentensi sahihi kisarufi***

A. Makaratasi mengi yamechomwa.

B. Mbuga la wanyama limefunguliwa.

C. Kuni ya kupikia imeletwa.

D. Kufuli la chuma limeuzwa.

27. Akisami $^{3}/_{7}$ kwa maneno ni

A. Theluthi saba

B sudusi tatu

C. Subui tatu

D. Thumni saba.

28. Chagua alama ya kufafanua zaidi

A. ;

B. :

C. /

D. -

29. ***Chagua karibu ya kiasi***

A. Karibu nianguke mtoni.

B. Amepewa karibu shilingi milioni moja.

C. Tunaishi karibu na shule.

D. Karibu hapa kwetu.

30. Kihisishi cha kukubaliana ni

A. Do!

B. Hewala!

C. Hamadi!

D. Huree!

Teacher.co.ke

**Soma taarifa ifuatayo kwa makini kisha ujibu maswali 31-40.**

Basi liliposimama nilishuka kama abiria wengine tukafululiza msalani kisha tukachukua nafasi zetu hotelini. Nilipenda sana sima na madondo, si kwa ladha yake ila kulingana na uwezo wangu kifedha. Nililetewa na kubugia kwa pupa. Nilipomaliza niliagiza pakiti ya mtindi na kugugumia kwa papawa.

Baada ya muda tukarejea garini. Tulingo'a nanga tena. Kitambo cha takribani robo saa tumbo likaanza kunichafuka. Nilihangaika na kula mumbi pale kitini. Jasho lilianza kunidondoka. Nilipozidiwa na dhiki, nilinyanyuka taratibu hadi kwa dereva. Nikamwomba kwa unyenyekevu asimamishe gari lakini badala yake alikanyaga kichapuzi.

Dereva alipuuza kabisa. Alihofia huenda nilikuwa mmoja wa wale wanaovizia magari barabarani. Wao huwa na mazoea ya kumtuma mmoja asafiri. Wenzake kuwa mahali fulani ambapo mwenzao ataomba basi lisimame aende haja. Dereva akilisimamisha gari pale alipoombwa, hao wenye nia mbaya hutoka vichakani na kuwahujumu abiria. Huwaumiza na kuwafilisi abiria, dereva na utingo.

Niliendelea kuhangaika bila mwombezi. Hatimaye dereva aliamua na liwe liwalo aliponiona nimefurama huku nimelowa jasho chapachapa. Aliliegesha basi kando ya barabara na kunipa nafasi ya kujisaidia. Sikungoja hata lisimame kabisa wala utingo kufungua mlango. Nilifungua himahima na kufyatuka nje kama risasi.

Hatimaye nilirejea basini na tukaendelea na safari. Niliposhushwa stanini nilichanganyikiwa nisijue kwa kwenda wala cha kufanya. Nilipokuwa nikitia na kutoa ili nijue hatua ya kwanza, vibako watatu wakaja shoti na kunipora kila kitu. Mkoba, stakabadhi hela na hata kunivua mavazi yangu. Niliachwa uchi wa mnyama katika eneo, nisilojua wa kunitilia upondo.

Laiti ningalikubaliana na rai za wavyele wangu za kuendelea na gange mashambani badala ya kwenda kubahatisha amali jijini. Kumbe waliosema kuwa asiyeonywa huona kwa macho yake walilenga ndipo.

31. Kulingana na aya ya kwanza basi lilitia nanga ili
A. abiria waingie mkahawani kushataki njaa
B. abiria waende pembeni kujisaidia
C. abiria wajisaidie kwa kula sima kwa mandondo
D. abiria wajisaidie kwa kushtaki njaa.

32. Msimulizi alikula ugali kwa maharagwe kwani
A. alikipenda sana chakula hicho
B. chakula hicho kilikuwa na ladha aliyoipenda
C. chakula hicho kililingana na hali yake ya kiuchumi
D. chakula hicho ndicho pekee kilichoandaliwa mkahawani.

33. Neno mtindi kama lilivyotumika katika taarifa lina maana gani?
A. Aina ya kinywaji cha matunda
B. Maziwa yaliyoganda
C. Namna ya kileo kikali
D. Maziwa yaliyotiwa katika pakiti.

34. Baada ya karibu dakika kumi na tano waliporejelea
A. msimulizi aliomba gari liegeshwe ajisaidie
B. msimulizi alilowa jasho chapachapa
C. tumbo la mnenaji lilianza kuvurugika
D. Dereva alikanyanga kichapuzi.

35. Dereva alifanya nini apoombwa kusimamisha gari?
A. Alisimamisha bila kukaidi ombi hilo
B. Alipuuza kuendesha basi kama awali
C. Hakuyasikia maneno yale kamwe
D. Aliongeza mwendo wa basi badala ya kufanya hivyo

36. Unafikiri abiria waliosafiri kwenye barabara zinazozungumziwa huhangaishwa na nani?
A. Majangili
B. Majambazi
C. Maharamia
D. Matapeli

37. Hatimaye msimulizi alishuka
A. basi liliposimama kabisa kwenye stendi
B. basi liliwa katika mwendo wa kasi
C. basi lilipowekwa kando ya barabara
D. basi lilipofunguliwa mlango na utingo

38. Kwa nini dereva alikata shauri kulisimamisha gari?
A. Alitambua hali ya mnenaji na kumwonea shutaka
B. Mnenaji aliendelea kutia tashliti
C. Basi lilikuwa limefika katika kituo kingine
D. Abiria walimwomba dereva kumhurumia mnenaji

39. Azma kuu ya msimulizi kutoka nyumbani ilikuwa
A. kutokana na uhaba wa kazi mashambani
B. kutamani amali za hadhi mjini
C. kuepuka rai na bughudha za wazazi wake
D. kuepuka kazi za sulubu mashambani

40. Kauli ya msimulizi katika sentensi ya mwisho wa taarifa inaonyesha kuwa
A. alisikitishwa sana na hali ya kuporwa kila kitu
B. alifadhaika sana maadamu hakujua yeyote mjini
C. alisikitika na kufedheheka sana moyoni
D. alijuta sana uamuzi aliofanya wa kuwakaidi wazazi.

Teacher.co.ke

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Ingawa mtihani ni muhimu mno katika mfumo wowote ule wa elimu, ni muhimu kutaja kwamba kwa sababu ya kusisitiza sana umuhimu wa mitihani, visa vya udanganyifu katika mtihani vimeshuhudiwa. Baadhi ya wanafunzi huhiaria kunakili majibu kutoka vitabuni ili kuipita mitihani yao na kujiunga na shule au vyuo mbalimbali.

Wazazi wengine huwalipa watu fulani kufanyia watoto wao mitihani. Hivi ni vitendo visivyokubalika. Mwaka uliopita waziri wa elimu aliweza kuziba mianya yote ambayo washikadau mbalimbali walitumia katika udanganyifu. Mashirika tofauti yalimvulia kofia kwa kuirudisha hadhi ya mtihani katika taifa letu.

Mitihani japo hupima uwezo wa mwanafunzi katika masomo fulani, hauwezi kutumiwa kama kigezo tosha cha kutathmini umilisi wa mwanafunzi. Wapo baadhi ya wanafunzi ambao ni hodari masomoni. Lakini huenda wasifanye vyema katika mtihani. Jambo hili huweza kusababishwa na hali ya afya ya mwanafunzi wakati wa mtihani, fadhaa au uchechefu wa karo. Baadhi ya watu ambao hawakufua dafu katika mitihani huenda wakawa watenda kazi wema.

Mitihani huhitaji matayarisho ya dhati. Mwalimu pia ana jukumu la kumsaidia mwanafunzi katika matayarisho na kuhakikisha kuwa amemwelekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na aina mbalimbali za maswali na jinsi ya kuutumia muda wake. Aidha mwalimu anahitajika kumshauri ni somo gani linalohitaji kushughulikiwa kwa makini zaidi. Ni muhimu pia mwalimu amshauri mwanafunzi kuhusu jinsi ya kudurusu na kujihusisha katika michezo mbalimbali ili kupumzisha akili. Juu ya haya yote ni muhimu mwanafunzi kujua kwamba anahitaji lishe bora ili kupata nguvu kuyatalii masomo na kuikabili mitihani yake.

Binadamu hana budi kufanya mitihani mbalimbali aushini mwake. Hata hivyo haifai kuichukua mitihani kama kibali cha kuwabagua watoto. Baadhi ya wanajamii huwadharau watoto wasiofanya vyema katika masomo yanayostahiwa na jamii hivyo. Watu kama hawa huwatia watoto kiwewe na kutojiamini. Wazazi wengine hata huwalazimisha watoto kusomea taaluma ambao wao wazazi wanazipendelea. Jambo hili huwafanya wana hawa kusagika kufanya masomo wasiyoyamudu vyema.

Wanaofanya vyema hushehenezwa sifa kochokocho mbele ya ndugu zao pasi kujali hisia za ndugu hao. Jambo hili huzua uhasama miongoni mwa ndugu, uhasama ambao usipoangamizwa huleta hasama katika familia. Hatuna budi kutumia mtihani kumkuza binadamu bali si kumviza.

41. Kulingana na aya ya kwanza
A. umuhimu wa mtihani huchangia sana visa vya udanganyifu
B. utiliaji mkazo katika umuhimu wa mtihani huchangia udanganyifu
C. wote wanaofuzu mtihani hawana budi kudanganya.
D. mitihani ndivyo njia ya pekee ya kutathmini maendedeleo.

42. Upi si udanganyifu katika mitihani?
A. Kupitia vitabu muda mfupi tu kabla ya mtihani
B. Kufanyiwa mtihani kwa kiasi fulani cha pesa
C. Kutafiti majibu vitabuni wakati wa mtihani
D. Kunakili jibu la swali gumu kutoka kwa mwanafunzi mwerevu.

43. Madhara makuu yanayotokana na udanganyifu katika mitihani unafikiri ni yapi?
A. Shule kutozwa faini na baraza la mitihani
B. Mwanafunzi kunaswa na kuadhibiwa vikali
C. Kupata matokeo murua ujanja unapogunduliwa
D. Kupoteza muda na mali wanafunzi wanapolazimika kurudia mtihani.

44. Kwa nini mtihani si kigezo bora cha kupimia umilisi?
A. Huku ni kuwapuuza wanafunzi dhaifu katika masomo
B. Mtihani huchukua muda mwingi na kuwachosha watahiniwa
C. Yapo masuala yanayoweza kuathiri matokeo hata ya mwanafunzi hodari
D. Wanafunzi wengi hawapendi kufanya mtihani wowote.

45. Neno fadhaa lina maana sawa na
A. wasiwasi
B. parapawa
C. huzuni
D. ghadhabu

46. Ni kweli kusema kuwa
A. watu wote walifuzu mitihani vizuri hufanya kazi vyema
B. watu wote waliofeli mitihani hawawezi kufanya kazi vyema
C. baadhi ya watu hujiangusha mitihani ili kupata kazi njema
D. baadhi ya watu waliofeli mitihani wanaweza kufanya kazi vyema

47. Jukumu kuu la mwalimu katika mtihani ni lipi
A. Kuteua majibu sahihi ili asiwaangushe wanafunzi wake
B. kumwandaa mwanafunzi kikamilifu kabla ya kukabiliana na mtihani
C. kumshauri mwanafunzi kuhusu njia mbadala za kupita mtihani
D. kumkashifu na kumtamausha mwanafunzi kabla ya kufanya mtihani

48. Kulingana na maelezo katika aya ya nne
A. michezo husaidia kupumzisha akili
B. lishe bora husaidia kupumzisha akili
C. michezo hutupatia nguvu za kuyatalii masomo
D. lishe bora husadia kuvinyosha viungo.

49. Mitihani huadhiri vipi uhusiano katika familia?
A. Watoto wengine hulazimisha kusomea taaluma wasizozimudu
B. Watoto hutiwa kiwewe na hali ya kutojiamini
C. Wasiofanya vyema hustahiwa na jamii zao
D. Huweza kuzua uhasama na kuleta uadui.

50. Mwandishi wa makala haya anaonelea kuwa
A. mtihani haufai katu; tutafute vigezo vingine muhimu
B. ni vigumu sana kukabiliana na udanganyifu katika mtihani
C. mtihani unaweza kumkuza au kumviza binadamu
D. mitihani imefaa sana kama kigezo cha kutathmini masomo.